



## Sintaksia Ya Kirai Kijalizo Na Uchopoaji Wa Viambajengo Katika Kiswahili

**Joseph Wanyonyi Mulalu, Mosol Kandargor & Mary Lonyangapuo**

*Moi University*

*Idara ya Kiswahili na lugha zingine za Kiafrika*

### IKISIRI

Kazi hii imeshughulikia sintaksia ya Kirai kijalizo (Kkijzo) na uchopoaji wa viima katika sentensi za Kiswahili. Viambajengo katika sentensi ya Kiswahili huweza kuchopolewa kutoka kiwango cha kirai wakati (Kwkt) na kutua katika kiwango cha Kkijzo. Kutokana na wingi wa dhima za viambajengo vinavyochopolewa na kutua katika kiwango cha Kkijzo, mbali na virai vya kidesturi vya Kkijzo kazi hii imependelekeza kupanuliwa kwa Kkijzo ili kijumuise virai vya ziada kama vile: Kirai arifu na Kirai kiwakilishi. Aidha kazi hii, imechunguza mofosintaksia ya

vijalizo changamano ndi- na amba- na kipatanisho kijalizo -o- kama vipashio vinavyotumika kuchopoa viambajengo katika sentensi za Kiswahili. Lengo hasa la utafiti huu ni kubaini nafasi zinazokaliwa na viambajengo hivi vya uchopoaji kwa mujibu wa muundo mzima wa sentensi zilizochopolewa. Uchanganuzi wa data katika karatasi hii utafanywa kwa kujikita kwa nadharia ya Kanuni Finyu hasa mapendelekezo ya hivi karibuni ya kigezo cha ugandaji wa kiima.

### ABSTRACT

*This work examines the syntax of the complement phrase (CP) and its relevance in extraction of elements in Kiswahili sentences. Elements in Kiswahili sentences can be extracted from the tense phrase (TP) to various positions within the CP. As a result of the various elements that land within the CP in a Kiswahili extracted sentence, this paper proposes the expansion of the CP beyond the traditional CP phrases so as to include additional phrases such as the: Pronoun phrase and Predicate phrase. This work also examines the morphosyntax of the Kiswahili complex complementizers ‘-amba’ and ‘ndi’ and the agreement complementiser -o- as elements that implement complementation in language under study. The aim of this paper is shade light on the positions occupied by these complementizers in relation to the structure of an extracted Kiswahili sentence. Data analysis is done based on the Minimalist theory specifically in line with the split CP hypothesis*

**Published:** 15<sup>th</sup> November 2017

**Disclosure statement:** No potential conflict of interest was reported by the author.

**To cite this article:** Wanyonyi Mulalu (2017) *Sintaksia Ya Kirai Kijalizo Na Uchopoaji Wa Viambajengo Katika Kiswahili*, Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences 1:9, 60-90, Full Terms & Conditions of access and use can be found at [www.royallitepublishers.com](http://www.royallitepublishers.com)

**Orcid ID:** <http://orcid.org/0000-0003-3729-5335>

## Maelezo ya alama zilizotumiwa

**KArifu** - Kirai kiarifu, **Kib** - Kibainishi, **Kfokasi** - Kirai fokasi, **Kijlzo** – Kijalizo, **KKIB** - Kirai kibainishi, **Kkiima** - Kirai kiima, **Kkirejeshi** - Kirai kirejeshi, **Kkiw** - Kirai Kiwakilishi, **Kmada** - Kirai mada, **KMZ** - Kanuni ya mchomozi ziada, **KN** - Kirai Nomino, **Knguvu** - Kirai nguvu, **Kswali** - Kirai swali, **Kt** - Kirai cha kitenzi chepesi, **Kwkt** - Kirai wakati, **Kukomo** - Kirai ukomo

## Utangulizi

Kwa mujibu wa *A Dictionary of Linguistics and Phonetics, sixth edition* (2008), ‘Uchopoaji ni istilahi inayotumika katika isimu kurejelea mchakato wa kisintaksia ambao husogea kiambajengo kutoka katika ‘kikundi’ (*unit*) fulani hadi nafasi fulani nje ya kikundi hicho husika (TY). Kwa mfano, inawezekana kuchopoa kiima katika sentensi ‘Yohana aliona simba’ na kupata sentensi zifuatazo:

- Ia. Yohana aliyeona simba
- b. Ni (Yohana aliyeona simba)

Ingawa ‘kikundi’ kinachozungumziwa hapo juu kinaweza kupewa ufasiri mbalimbali, katika kazi hii istilahi ‘kikundi’ itarejelea kirai wakati (Kwkt). Kwa hivyo, katika kazi hii, uchopoaji ni mchakato wa kisintaksia unaosogea viambajengo vinavyotokea katika kiwango cha Kwkt hadi kiwango/ulingo wa Kirai kijalizo (Kkijzo) au hata katika vishazi vingine vinavyota juu ya kishazi ambacho kwacho kiambajengo kinachopolewa. Katika nadharia ya Kanuni Finyu, ulingo wa Kkijzo cha sentensi (nafasi iliyo juu ya Kwkt na kabla ya kishazi kingine cha juu) hurejelewa kama **ukingo wa kushoto** mwa sentensi. Kwa hivyo viambajengo vya sentensi vilivyochopolewa husemekana kuwa vimesogezwa hadi ‘ukingo wa kushoto’ wa sentensi au juu zaidi hadi kishazi kingine kinachotokea juu ya ‘ukingo wa kushoto’ wa kishazi cha chini. Kwa mfano, katika sentensi ya Ia, KN ‘Yohana’ kimesogezwa kutoka nafasi yake katika Kwkt hadi kwenye ‘ukingo wa kushoto’ wa sentensi kuitia uchopoaji huku kiambajengo hiki kikiwa kimesogezwa hadi kwenye kishazi kinachotokea juu ya ‘ukingo wa kushoto’ wa sentensi katika Ib. Karatasi hii imejikita katika kuhoji muundo wa ukingo wa kushoto kwa lengo la kuibua nafsi zaidi za utuaji wa viambajengo vilivyochopolewa kama inavyotokea katika lugha inayotafitiwa.


## Nafasi za Kidesture za Kirai Kijalizo Kilichogawanywa

Ukingo wa kulia wa sentensi kwa muda mrefu umekuwa ukirejelewa kidesturi kama uwanja wa kirai kijalizo (Kkijzo) kutokana na sababu kuwa neno kuu la kirai hiki huwa kijalizo. Ni kutokana na nafasi inayokaliwa na kijalizo katika sentensi ndipo ikaja kuaminika kuwa neno kuu la kirai kinachokuja juu ya Kwkt huwa ni kijalizo. Kijalizo katika lugha kama Kiswahili na Kiingereza kwa kawaida huja kabla ya viima vya vishazi vinavyoteuliwa na vijalizo husika. Radford (2009) anadai kuwa kijzo, neno kuu la Kkijzo hujazwa na maneno makuu kama vile: ikiwa, kuwa, je na kwamba kama inavyotokea katika mazungumzo yafuatayo:


2. Mnenaji A: Kuna kitu nimekuwa nikitaka kukuuliza kwa mda mrefu mpenzi.  
Mnenaji B: Ni nini barafu yangu ya moyo?
- Mnenaji A: **Ikiwa utanioa**  
Mnenaji wa B: (*Akijitia hamnazo kuwa hajasikia*) Unasema nini mpenzi?  
Mnenaji wa A:**Je, utanioa?**

Katika mazungumzo haya, sentensi katika wino uliokolezwa ni mfano wa miundo iliyo na kijzo. Katika mifano hii msamiati ‘ikiwa’ na ‘je’ ni vijalizo. Miundo ya sentensi hizi ikiwa ifuatayo:

3a. Ikiwa utanioa



b. Je, utanioa?




Kutokana na mifano hii, inabainika kuwa mchomozo wa juu kabisa wa kishazi ni Kkijzo, hali inayofanya kishazi ukomo kuwa na muundo wa michomozo mitatu ya kimsingi; Kkijzo, Kwkt na KT kama inavyobainishwa na wino uliokolezwa katika vielelezo vya 3a na b. Hata hivyo sentensi zifuatazo zinazua changamoto kwa ufasiri wa Kkijzo kama wenye mchomozo mmoja tu.

4a. Mtihani utatangazwa kesho

b. Kesho mtihani utatangazwa


c. Mwalimu alisema (kwamba kesho mtihani utatangazwa)

Katika mifano hii, mfano wa 4a ni kishazi kisoukomu na kwa hivyo muundo wake una mchomozo wa juu kabisa wa Kkijzo ambacho kina neno kuu ‘kijzo’ ambalo ni tupu kifonolojia huku katika mfano wa 4 b nafasi hii ya neno kuu la Kkijzo imejazwa na neno ‘kesho’ muundo wake ukiwa;



Ingawaje, kuna utata wa uwakilishaji wa Kkijzo unatokea katika sentensi ya 4c ambapo viambajengo vilivyopigiwa mstari katika kishazi kwenye mabano vinatokea katika kiwango cha Kkijzo. Viambajengo hivi vyote ni maneno makuu yenyen uamilifu tofautitofauti na kwa hiyo hayawezi kukalia nafasi moja ya kijzo katika muundo wa Kkijzo. Swali ni je, ni vipi tuwakilishe muundo wa Kkijzo cha kishazi kama hiki?

Kutokana na changamoto za uwakilishaji wa Kkijzo cha kishazi kama hiki kilicho katika mabano katika sentensi ya 4c, Rizzi (1997, 2001b na 2004) amependekeza kuwa Kkijzo sharti kigawanywe katika michomozo mingine kadhaa, hali inayorejelewa kama nadharia ya ugawanyaji wa Kkijzo. Kulingana na Rizzi, vijalizi kama vile; ikiwa, kuwa, je, sababu na ala!, kutokana na dhima yao ya kubaini iwapo kishazi ni swali, amri, mshangao au arifu, vinachanganuliwa kama vibainishi nya nguvu za kishazi na kwa hivyo ni maneno makuu ya kirai nguvu (Knguvu). Kwa upande mwingine, viambajengo vilivyochopolewa kama vile ‘kesho’ katika mfano wa 4b na c vinatokea kama vibainishi nya kirai fokasi (KFokasi). Chagizo ‘kesho’ kimechopolewa kutoka nafasi ya ndani ya KT hadi kiwango cha Kkijzo kama njia ya kukihimiza au kukturilia fokasi. Kwa mujibu wa maelezo haya, muundo wa Kkijzo cha kishazi katika mabano katika sentensi ya 4c ‘kwamba kesho mtihani ukatangazwa’ ni ufuatao:




Mbali na Kfokasi, uchopoaji wa viambajengo unaweza kusogezwa hadi katika ulingo wa Kkijzo kwa lengo la kukifanya mada ya kishazi. Nafasi ambapo mada hutua katika muundo wa Kkijzo kilichogawanywa kwa mujibu wa Rizzi ni kirai mada (Kmada). Mfano ufuatao unaweza kutumika kijadili suala la Kmada.

#### 7.a Hatutavumilia tabia kama hiyo kamwe

b (Tabia kama hiyo)<sub>i</sub> hatutaivumilia kamwe t<sub>i</sub>

Katika mifano wa 7b, kiambajengo ‘tabia kama hiyo’ kimechopolewa kutoka nafasi ya kijalizi cha kitenzi ‘vumilia’ ambapo sentensi kamili kabla ya kuchopoa yambwa hii ni ile sentensi ya 7a. Muundo wa Kkijzo cha sentensi ya 7b ukiwa:



Swali ni je katika sentensi yenye viambajengo viwili vilivyochopolewa kama inavyobainika katika sentensi ifuatayo ya 9, ni vipi tuamue kiambajengo gani kinasogezwa hadi Kfokasi na kipi kisogezwe hadi Kmada? Vinginevyo ni kuwa, ni nini tofauti kati ya Kfokasi na Kmada?

9. Kuwa tabia kama hiyo, kesho, hatutaivumilia kamwe t<sub>i</sub> t<sub>k</sub>.

Radford (2009) amependekeza kipimo cha upya/ukuukuu wa habari kimuktadha katika kutofautisha kati ya fokasi na mada. Kmada husheheni viambajengo ambavyo vinabeba ujumbe ambao unajulikana tayari kimuktadha huku Kfokasi kikiwa kiambajengo kinachobeba habari ambazo ni mpya kabisa kimuktadha. Tunaweza kubainisha tofauti kati ya Kfokasi na Kmada kwa kutumia muktadha wa mazungumzo kati ya A na B ifuatavyo :

10. A : Wanafunzi walipigana na kung'ang'ania chakula leo jioni.


B : Tabia kama hiyo, kesho, sitaivumilia kamwe.

(Baadaye jioni hiyo, B alipokutana na c)

C : B alisema nini ulipomwambia habari ya wanafunzi?

B: Kuwa, tabia kama hiyo, kesho, hataivumilia kamwe.

Katika muktadha wa mazungumzo haya, kiambajengo 'kesho' ni habari ngeni huku 'tabia kama hiyo' ni habari ambayo tayari inajulikana kimuktadha kwani inarejelea 'ku<sup>p</sup>igana na kung'ang'ania chakula kwa wanafunzi'. Kwa hivyo katika mazungumzo ya B katika 10, na katika sentensi ya 9, kipashio 'kesho' ni Kib cha Kfokasi huku 'tabia kama hiyo' nacho kikiwa kibainishi cha Kmada. Kwa mujibu wa Rizzi (1997) kimuundo, Kfokasi hutokea juu ya Kmada, na chini ya Knguvu. Kwa hivyo, muundo wa kishazi cha pili kutamkwa na B utakuwa ufuatao:



Radford (2009 : 326) naye ametumia sentensi ifuatayo ya 12 kubainisha utokeaji wa Kmada, Knguvu na Kfokasi katika muundo wa Kkijzo.


12 a. He prayed that *atrocities like those, never again would he witness*.

Aliomba kuwa ukatili kama huo, siku nyingine, asiushuhudie tena.

b. \*He prayed that *never again, atrocities like those would he witness*.

Aliomba kuwa siku nyingine, ukatili kama huo, asiushuhudie

Katika sentensi hii, viambajengo katika hati mlazo ni Kkijzo chenye kiambajengo ‘that’ - kikiwa sehemu ya Knguvu, ‘*atrocities like those*’- Kmada na ‘*never again*’- Kfokasi. Muundo wa sentensi ya 12 a ya Kiingereza ukiwa ufuatao :




Ushahidi kuwa Kmada huja juu ya Kfokasi katika muundo wa Kkijzo unatokana na sentensi ya 12b ambapo mpangilio wa viambajengo unaoweka Kfokasi juu ya Kmada unakataliwa kisarufi. Hata hivyo deta ya Kiswahili ina ushahidi kinyume. Katika lugha hii, inabainika kuwa kuna uhuru wa wazungumzaji wa lugha hii kuweka Kmada kabla au baada ya Kfokasi ambapo mbali na sentensi ya 9, sentensi ifuatayo hapo chini ya 14 vilevile inakubalika kisarufi licha ya kupangua mpangilio wa viambajengo na kuweka Kfokasi kabla ya Kmada.

#### 14. Kuwa kesho, tabia kama hiyo hatuataivumilia.

Kutokana na changamoto zinazotokana na lugha kama vile Kiswahili, kama ilivyo katika sentensi ya 14 ambapo Kfokasi huja juu ya Kmada, Rizzi (1997) amependekeza mfumo ufuatao wa virai katika muundo wa Kkijzo kilichogawanywa ambapo Kfokasi kinaweza kutokea juu au chini ya Kmada:

15.



Muundo huu unakadiria hali ambapo Kfokasi kila mara hutokea chini ya Kmada kama ilivyo katika Kiingereza na hali ambapo Kfokasi kinaweza kutokea kwa hiari juu au chini ya Kmada kama ilivyo katika lugha kama Kiswahili.

Hadi hapa, imebainika kuwa Kkijzo kinachotokea juu ya Kwkt kinaweza kugawanya katika michomozo midogo ya Knguvu, Kmada na Kfokasi. Hata hivyo, Rizzi anapendekeza kuwa chini ya Kfokasi au Kmada kutegemea kirai kinachokuja chini ya kingine na juu ya Kwkt, kuna mchomozo wa nne wa Kirai ukomo (Kukomo) kilicho na neno kuu ukomo lenye uamilifu wa kubaini iwapo kishazi husika ni ukomo au kisoukomo. Kwa kutumia mfano wa lugha ya Kitaliano, Rizzi anasema kuwa ukomo ni nafasi inayokaliwa na kijalizo *di* sawia na ‘for’ cha Kiingereza. Kihusishi hiki, katika lugha hii hutumika kuingiza kishazi kisoukomo katika muundo kama ilivyo katika mfano ufuatao ;


16. Gianni pensa, *il tuo libro*, di KIW cononsierlo bene [ Rizzi 1997 : 300]

Gianni anafikiria Kib chako kitabu di KIW kukijua vizuri

Gianni anafikiria kitabu chako, anakijua vizuri

Kwa mujbu wa Rizzi, kishazi katika hati mlazo katika sentensi ya 16 ni kijalizo cha kitenzi *pensa* (anafikiria) na kishazi hiki kina muundo uliosahilishwa ufuatao :

17.



Katika muundo huu, *il tuo libro* (kitabu chako) ni ‘mada’ huku *di* (kwa) ni neno kuu la ukomo ambalo hubainisha kishazi husika kama kisoukomo.

Rizzi (1997) anasema kuwa ingawa katika Kiingereza, ilifikiriwa kuwa vijalizo kama vile ‘that’ na ‘for’ vilikalia nafasi moja ya Kkijzo katika muundo wa kishazi, kuna miundo katika lugha hii inayodhibitisha kuwa vijalizo hivi hukalia nafasi tofauti katika Kkijzo kilichogawanywa. Mifano ifuatayo ni baadhi ya miundo hii:

- 18a. He is anxious [that John should leave tomorrow] [ Rizzi 1997 : 301]
- b. He is anxious [that tomorrow John should leave]
- c. He is anxious [for John to leave tomorrow]
- d.\*He is anxious [for tomorrow John to leave]

Katika mifano hii, kielezi cha wakati kinapochopolewa kama ilivyo katika 18b na c, hutua katika nafasi ya Kfokasi. Katika muundo wa Kkijzo kilichogawanywa, kijalizo ‘that’ kama kilivyo katika mfano wa 18a na b hukalia nafasi ya Knguvu ambacho huja juu ya Kfokasi. Sentensi ya 18b inakubalika kwa sababu muundo wake unapatana na maelezo haya. Tunatarajia sentensi ya 18d vilevile kukubalika kisarufi iwapo kijalizo ‘for’ katika 18c na d vina uamilifu sawa na ‘that’ katika mfano wa 18a na b. Hata hivyo, kukataliwa kwa sentensi ya 18d baada ya kuchopoa kielezi cha wakati ‘tomorrow’ kunaashiria kuwa huenda kijalizo ‘for’ si Knguvu na kwamba nafasi yake katika muundo iko chini ya Kfokasi. Kufuatia mfano huu, Rizzi (1997) anadai kuwa kijalizo ‘for’ kama kinavyotumika katika Kiingereza vilevile kina uamilifu wa neno kuu la Kukomo na kwa hivyo nafasi yake katika muundo wa Kkijzo kilichogawanywa iko chini ya Kfokasi. Ni kunatokana na sababu kuwa sentensi ya 18c inaweka kiambajengo ‘for’ ambacho ni Kukomo juu ya Kfokasi kinyume na muundo wa kidesturi wa Kkijzo kilichogawanywa ndipo sentensi hii inakataliwa kisarufi.

Kwa huhitimisha, tunaweza kusema kuwa Kkjizo kinaweza kugawanywa katika michomozo minne ya kidesturi ya Knguvu, Kfokasi, Kmada na Kukomo. Baada ya kuelewa huu muundo wa Kkijzo kilichogawanywa, hebu sasa tuangalie umuhimu wa muundo huu katika uchopoaji wa viima katika sentensi za Kiswahili.

### **Mofosintaksia ya Uchopoaji wa Viambajengo katika Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili sawia na lugha zingine ulimwenguni hudhahirisha hali ya uchopoaji wa viambajengo katika sentensi zao. Uchopoaji wa viambajengo katika Kiswahili huwezeshwa na vijalizo changamano ‘amba-kpt-o’, ‘ndi-kpt-o’ na kipatanishi kijalizo ‘-o’ kinachotokea kama kiambishi kwenye kitenzi. Sehemu hii itachunguza mofosintaksia ya hivi viambajengo vinavyowezesha uchopoaji wa viambajengo vingine katika sentensi kwa lengo la kubaini mofolojia na sintaksia yake.

Lugha ya Kiswahili huweza kuchopoa viima vyake kama inavyobainika katika sentensi zifuatazo:

- 19 a. Watoto walinunua mkate
- b. Watoto walionunua mkate
- c. Watoto **ambao** walinunua mkate
- d. Watoto **ndio** walionunua mkate

Sentensi ya 19a ni sentensi arifu. Kutokana na sentensi hii, kunaweza kuunda aina mbalimbali ya vishazi au sentensi kuitia uchopoaji wa kiima cha sentensi hii ya 19a. Kutokana na huu uchopoaji, kiima katika muundo kimetua katika sehemu mbalimbali ya

**ukingo wa kulia** kwa mujibu wa muundo wa Kkijzo kilichopanuliwa cha Rizzi (1997, 2001b na 2004) na Radford (2009) na kuzalisha aina mbalimbali ya vishazi vikiwemo vishazi virejeshi na sentensi teguzi mada.

Mbali na uchopoaji viima, Kiswahili vilevile kinaweza kuchopoa viambajengo visivyokuwa viima. Katika mfano wa 20, unaotokana na sentensi ya 19a hapo juu, tumeonyesha namna uchopoaji wa yambwa unavyotokea katika lugha hii:

- 20 a. Mkate walionunua watoto
- b. Mkate **ambao** watoto walinunua
- c. Mkate **ndio** watoto walinunua

Kwa mujibu wa data hii ya 19 na 20, mchakato wa uchopoaji wa viambajengo katika Kiswahili hutumia mbinu kadha zikiwemo: kijalizo **amba-**, kijalizo **ndi-** na **o-** rejeshi. Sehemu inayofuata imeangazia mofosintaksia ya vijalizo **amba-** na **ndi-** na **-o-** rejeshi katika sentensi za Kiswahili.

### **Asili ya Vijalizo vya Uchopoaji ‘amba-’ na ‘ndi-’**

Katika kujadili mofosintaksia ya vijenzi hivi vya sentensi, ni muhimu kutambua kuwa hivi si viambajengo vya pekee ambavyo vinaweza kuainishwa kama vijalizo katika lugha inayotafitiwa. Lugha hii ina vijalizo vingine kama: kama, kwamba, kuwa, ijapokuwa na ikiwa kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

- 21 a. Wanafunzi walipata habari **kwamba** wahadhiri wange goma Jumatatu
- b. Juma anasema **kuwa** atafikisha ujumbe huo kesho mapema

Licha viambajengo hivi kutokea katika ulingo wa Kkijzo cha Kiswahili na kwa hivyo kuwa na uamilifu wa vijalizo sawia na vijalizo ‘amba-’ na ‘ndi-’, viambajengo hivi hutofautiana kimofolojia na kisintaksia. Kwanza ni kuwa kiuamilifu, vijalizo vinavyotokea katika sentensi ya 21 ni viarifu huku vijalizo ‘amba-’ na ‘ndi-’ vikiwa na uamilifu wa kuchopoa viambajengo. Pili kimofolojia, aina ya vijalizo vinavyotokea katika sentensi ya 21 vinaweza kurejelewa kama vijalizo sahili kwani vinaundwa kutokana na mofimu huru. Kwa upande mwingine, vijalizo ‘amba-’ na ‘ndi-’ ni changamano kutokana na hali kuwa vimeundwa kutokana na zaidi ya mofimu moja: yaani mzizi ‘amba-’ ama ‘ndi-’, ukifuatwa na kipatanishi cha nomino iliyocho polewa na kisha kiambishi ‘o’. Katika sehemu iliyo salia ya kazi hii tutarejelea kijalizo ‘amba-’ kama ‘amba-kpt-o’ huku kile cha ‘ndi-’ kikirejelewa kama ‘ndi-kpt-o’ kutokana na mofolojia yao. Miundo changamano ya vijalizo ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’ inazua maswali yafuatayo ambayo yanahitaji kufafanuliwa:

Ni nini uamilifu wa mizizi ‘amba-’ na ‘ndi-’?

Ni nini uamilifu wa kiambishi ‘-o’ kisichobadilika kinachotokea kama kiambishi tamati katika vijalizo changamano ‘amba-’ na ‘ndi-’? (ni upatanishi ndio hubadilika na wala si ‘o’)

Je, vijalizo ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’ vinakalia nafasi gani katika ukingo wa kushoto mwa sentensi au kishazi ?


Tunawajibikia vipi upatanishi unaoshuhudiwa kati ya vijalizo hivi na nomino iliyochopolewa. Hasa, ikizingatiwa kuwa kiambishi hiki hutokea kama kiambishi tamati kwa mujibu wa mzizi wa vijalizo hivi kinyume na vilivyo viambishi vipatanishi vya kidesturi vinavyotokea kama viambishi awali katika lugha hii?


Ili kujadili kikamilifu masuala haya, tumependekeza nadharia tete kadhaa ambazo tumezitumia kuangazia masuala haya muhimu tuliyoyazua huku tukitathmini kila nadharia kwa kuonyesha udhabit na udhaifu wake.

Pendekezo letu la kwanza ni kuwa ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’ vyote huingiza na kukalia nafasi ya neno kuu la Knguvu sawa na vijalizo sahili; ‘kuwa’, ‘ikiwa’ na ‘kwamba’ za lugha hii na ‘that’ ya Kiingereza kama anavyopendekeza. Pendekezo hili ni muhimu kwa vile linatuwezesha kuonyesha usawa uliopo kati ya hivi vijalizo changamano na vile vilivyo sahihi kwani vyote vinatuwezesha kubaini aina ya vishazi yaani iwapo ni; virejeshi, arifu, swali au teguzi. Pendekezo hili hata hivyo, lina dosari moja kubwa kwani linaonekana kutozingatia ukweli kwamba vijalizo hivi vimeundwa kutokana na vipashio vitatu vya kimofolojia. Hivyo basi, pendekezo hili linafunika ukweli kuwa vijalizo hivi ni changamano kwani vina mofimu tatu. Ni hizi mofimu ndizo tunazolenga kuonyesha uamilifu wake na kwa hivyo mwelekeo huu wa fikra hautufikishi mbali kwa mujibu wa malengo yetu ya hapo juu.

Nadharia tete ya pili inarejelea michomozo iliyomo katika ulingo wa kijalizo kwa mujibu wa Rizzi (1997) kama ilivyo katika kielelezo cha 15 hapo juu. Vipashio ‘amba-’ na ‘ndi-’ na ‘o’ katika vijalizo changamano ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’ havibadiliki. Kinachobadilika ni vijatanisho inavyopatanisha vijalizo hivi na nomino zilizochopolewa. Hali hii inatuelekeza kufikiria kuwa viambajengo ‘amba-’ na ‘ndi-’ na ‘o’ ni maneno makuu ya aina fulani. Aidha kwa vile vipashio hivi ni vijalizo vya aina moja au nyingine, tunaweza kusema kuwa haya maneno makuu yanapatikana katika sehemu ya ukingo wa kushoto mwa sentensi. Lakini swali ni je, haya maneno makuu yanatokea katika michomozo gani katika ukingo wa kushoto wa sentensi?

Nadharia tete ya pili inadai kuwa vipashio ‘ndi-’ na ‘amba-’ ni maneno makuu ya Kfokasi huku ‘o’ ikiwa neno kuu la Kmada au vinginevyo ni kuwa ‘o’ ni neno kuu la Kfokasi huku ‘amba-’ na ‘ndi-’ yakiwa maneno makuu ya Kmada. Muundo wa maneno makuu haya yaitokea katika mfumo wa kijalizo utakuwa 22a au 22b kutegemea ni kirai gani kinachokuja juu ya kingine katika muundo:





Umuhimu wa pendekezo hili ni kuwa kwa kutumia nafasi zilizomo tayari katika muundo, tumeonyesha kuwa vijalizo ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’ ni changamano na kuwa kila kipashio kina dhima maalumu katika muundo mzima.

Hata hivyo, miundo ya 21a na b inajikuta katika utata vilevile, suala la aina ya kishazi/ sentensi linapoingizwa katika uchunguzi wa miundo hii. Kuna baadhi ya vishazi/sentensi ambazo zinadhihirisha kuwa Kmada na Kfokasi haviwezi kutokea pamoja katika muundo. Hebu tuchunguze sentensi zifuatazo ambazo ni zao la vijalizo ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’:

- 23 a. Nini ndicho kilichogonga nyumba (*swali teguzi*)  
 b. Nini ambacho kiligonga nyumba(*swali lililochopoa kiima kiulizi*)  
 c. Gari ndilo lililogonga nyumba (*sentensi teguzi*)  
 d. Gari ambalo liligonga nyumba (*kishazi kirejeshi kiima*)  
 e. Nyumba ambayo gari liligonga (*kishazi kirejeshi yambwa*)


Mifano ya 23a na b ni maswali yaliyo na viwakilishi viulizi vilivyopigiwa mistari. Sentensi za swalî hazina Kmada katika muundo wake na kwa hivyo haitakuwa sahihi kudai kuwa ama ‘ndi-’ au ‘amba’ au ‘o’ huingizwa katika muundo kama neno kuu la Kmada katika mifano hii. Aidha, mifano wa 23c ni sentensi teguzi ambayo kiima cha kishazi cha chini kimechopolewa hadi nafasi ya Kfokasi. Nadharia tete yetu hii vilevile inakabiliwa na matatizo katika sentensi hii ya 23c kwa vile katika aina hii ya sentensi hakuna mchomozo wa Kmada ambao unaweza kukaliwa ama na neno kuu ‘ndi-’ au ‘o’ ya kijzo ‘ndi-kpt-o’.

Mifano ya 23d na e vilevile inakabiliwa na matatizo yayo hayo tuliyobainisha hapo juu. Mifano hii inahusisha vishazi virejeshi. Muundo wa ulingo wa kijalizo cha vishazi virejeshi, ingawa una Kmada hauna mchomozo wa Kfokasi. Kwa hivyo si kweli kudai kuwa ama ‘amba’ au ‘o’ huingizwa katika muundo kama neno kuu la Kmada. Ushahidi huu kwa hivyo, inatuelekeza kutupilia mbali hili pendekezo la pili.

Pendekezo la tatu ni kuwa kiambishi ‘o’ katika vijalizo ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’ ndicho hutokea kama neno kuu la Knguvu huku maneno makuu ‘amba-’ na ‘ndi-’ yakiingizwa katika muundo katika nafasi iliyo juu ya Knguvu. Pendekezo hili linapatana na mwelekeo wa fikra wa Rizzi (1997) kuhusu vishazi virejeshi ambapo anadai kuwa opareta ya urejeshi husoga hadi sehemu ya Kib cha Knguvu. Katika hali hii, opareta hii ni nomino iliyochopolewa katika kishazi kirejeshi. Aidha, Henderson (2005) anapendekeza kuwa sifa za

urejeshi huzalishwa katika neno kuu la Knguvu. Kwa mujibu wa pendekezo hili, muundo uliosahilishwa wa kishazi kirejeshi kama vile cha 23d, kwa mfano, utakuwa ufuatao:

### 23 f. Gari ambalo liligonga nyumba




Licha ya pendekezo hili kupatana na fikra za baadhi ya wanaismu wakiwemo Rizzi (1997) na Henderson (2005), linakabiliwa na upungufu ikizingatiwa kuwa neno kuu la Knguvu (katika wino uliokolezwa) huamua aina ya kishazi yaani iwapo ni swali, kishazi rejeshi au sentensi arifu. Ikiwa tutachukulia kuwa vishazi vya aina mbalimbali huchukua kiambishi'-o' kama neno kuu la Kmada, tutashindwa kuwajibikia namna hii '-o' ileile moja inavyotumika kubaini nguvu za vishazi mbalimbali. Vinginevyo ni kuwa ni vipi tutatofautisha '-o' ya swali, kishazi rejeshi au sentensi arifu. Utokeaji wa '-o' katika nafasi hii unaonyesha kimakosa kuwa vishazi vyote vinavyochukua vijalizo 'amba-kpt-o' na 'ndi-kpt-o' ni vya aina moja kinyume na ilivyo katika mifano ya 23 hapo juu ambapo sentensi/vishazi hivi ni vya aina mbalimbali. Aidha, Knguvu kinachoamua aina ya kishazi huwa ndio upeo wa juu zaidi katika muundo wa kishazi. Hali hii, kwa hivyo, inazua utata wa kuwajibikia aina ya kirai cha X (KX) ambacho huchukua 'amba-' kama neno lake kuu ilhali kirai kizima kinatambulika kiupeo kama kishazi kirejeshi. Kwa misingi hii, tunapitisha hukumu kuwa nadharia tete hii ya tatu vilevile haina mashiko.

Katika pendekezo la nne, utafiti huu utafuata mwelekeo wa fikra ya Wasike (2007) aliposhughulikia kijalizo changamano 'hi-kpt-o' katika lugha ya Kibukusu. Kulingana na mawazo yake Wasike, vijalizo kama vile vya 'amba-kpt-o' na 'ndi-kpt-o', vina maneno makuu amilifu: 'amba-' na 'ndi-' ambayo huingizwa katika muundo kama (KAriku) kutokana na dhima yao ya kisemantiki ya kutumika kufafanua nomino zilizochopolewa. Kwa mujibu wa Wasike aidha, kipashio '-o' ni neno kuu la kiwakilishi (Kkiw) kutokana na dhima yake ya urejelesi wa kitu au vitu ulimwenguni sawa na ilivyo katika viwakilishi vionyeshi vya mbali kidogo kwa mfano; **huyo**, **hicho** na **hilo**. Jedwali lifuatato limebainisha mshabaha huu katika ngeli zote za Kiswahili:


### Jedwali 1: Utokeaji wa vijalizi 'ndi' - na 'amba' - na vionyeshi mbalimbali

<b>Ngeli</b>	<b>Mifano ya nomin o</b>	<b>Utokeaji na 'ndi'</b>	<b>Utokeaji na 'amba'</b>	<b>Utokeaji na viambishi vionyeshi vya mbali kidogo</b>
1	<b>mtoto</b>	<b>ndiye</b>	<b>ambaye</b>	<b>huyo</b>
2	<b>watoto</b>	<b>ndio</b>	<b>ambao</b>	<b>hao</b>
3	<b>mti</b>	<b>ndio</b>	<b>ambao</b>	<b>huo</b>
4	<b>miti</b>	<b>ndiyo</b>	<b>ambayo</b>	<b>hiyo</b>
5	<b>jino</b>	<b>ndilo</b>	<b>ambalo</b>	<b>hilo</b>
6	<b>meno</b>	<b>ndiyo</b>	<b>ambayo</b>	<b>hayo</b>
7	<b>kitanda</b>	<b>ndicho</b>	<b>ambacho</b>	<b>hicho</b>
8	<b>vitanda</b>	<b>ndivyo</b>	<b>ambavyo</b>	<b>hivyo</b>
9	<b>nyumba</b>	<b>ndiyo</b>	<b>ambayo</b>	<b>hiyo</b>
10	<b>Kuta, nyuzi</b>	<b>ndizo</b>	<b>ambazo</b>	<b>hizo</b>
11/14	<b>Ukuta, uzi</b>	<b>ndio</b>	<b>ambao</b>	<b>huo</b>
15/17	<b>kuimba</b> Shambani-kuna	<b>ndiko</b>	<b>ambako</b>	<b>huko</b>
16	Shambani - pana	<b>ndipo</b>	<b>ambapo</b>	<b>hapo</b>
18	Shambani - mna	<b>ndimo</b>	<b>ambamo</b>	<b>humo</b>

Kwa vile maneno makuu amilifu ya KArifu 'ndi-' na 'amba-' pamoja na Kkiw 'o' hutokea katika ukingo wa kushoto wa kishazi na kutokana na sababu kuwa Knguvu lazima kisalie katika muundo kama mchomozo amilifu wa juu zaidi katika ukingo wa kushoto (Rizzi 1997), Wasike (2007) anapendekeza kuwa KArifu na Kkiw hutokea kati ya Knguvu na Kfokasi. Katika Kiswahili, ni pendekozetu kuwa kirai kinachokuja chini ya KArifu kinaweza kuwa Kfokasi au Kmada kutegemea aina ya kishazi au nguvu ya kishazi husika. Muundo wa Kkijzo cha mfano wa 23a wa swali lililoteguliwa utakuwa ufuataeo:



Kwa upande mwingine, mfano wa 23e wa kishazi kirejeshi yambwa kina muundo ufuatao:



Katika miundo hii, kwa mfano muundo wa 24a, kiwakilishi kiulizi ‘nini’ hutua katika nafasi ya Kfokasi baada ya kuchopolewa kutoka Kwkt kisha kinanyanyuliwa hadi sehemu ya Kib ya Kkiw kutokana na sifa dhabiti ya nomino ya neno kuu la kirai hiki. Kikiwa katika nafasi hii na kupitia kwa upatanishi wa kuelekea juu, neno kuu ‘o’ huingia katika upatanishi na kiwakilishi kiulizi ‘nini’. Kisha kiwakilishi kiulizi hiki husogea hadi Kib cha KArifu. Kwa upande mwingine neno kuu la Kkiw pamoja na kiambishi kipatanishi chake husogea na kujiambisha kwenye neno kuu la KArifu kwa misingi kuwa viwili hivi ni viambishi na kwa hivyo lazima vitafute mwenyeji wao ambapo kwa pamoja vyote hivi vinatamkwa kama neno moja. Ni katika hatua hii ndipo viambishi hivi hujambisha kwenye neno kuu la KArifu ‘ndi’ na kutokea kama viambishi tamati vya msamiati ‘ndi-cho’. Hatimaye, kiwakilishi kiulizi husogea tena na kutua katika nafasi ya Kib cha Knguvu kutokana na sifa dhabiti za swali za Knguvu katika kishazi cha aina hiki cha swali. Katika kielelezo cha 24b aidha hatua zizi hizi za 24a hujirudia.

Nadharia tete hii ya nne ina faida zifuatazo dhidi ya nadharia zingine za awali:

- i. Inawajibikia upatanishi unaotokea kama viambishi tamati katika umbo la vijalizo changamano ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’.
- ii. Inafafanua dhima mbalimbali za mofimu/ viambishi katika vijalizo changamano ‘amba-kpt-o’ na ‘ndi-kpt-o’.
- iii. Inawajibikia Knguvu kama upeo juu zaidi katika kishazi na ambao hutambulisha aina ya kishazi yaani ikiwa ni swali, kirejeshi au aina nyingine yoyote ya kishazi.

Mwisho, ni muhimu kuwajibikia tofauti kati ya kijalizo ‘amba-’ na ‘ndi-’ kwani ilivyo ni kuwa kuna baadhi ya vishazi ambavyo hukubali kutokea na kijzo cha aina moja na kukataa aina nyingine. Kwa mfano, katika mfano wa 23, kijzo ‘amba-’ kinapoingizwa katika muundo kinapatana na nguvu kishazi cha swali au urejeshi. Kwa upande mwingine, kijzo ‘ndi-’

kinapotumika kuchopoa viambajengo, matokeo huwa vishazi teguzi au swali teguzi na wala si vishazi virejeshi. Ni vipi tuwajibikie hali hii kimuundo ilhali tumependekeza kuwa hivi vijalizo vinakalia nafasi sawa katika muundo yaani Kkiw na KArifu? Suluhisho letu kwa pendekezo hili limejikita kwa uteuzi zuivu wa kirai cha kiupeo yaani Knguvu. Knguvu kikiwa na nguvu ya kishazi teguzi kwa mfano huwa na uteuzi zuivu wa kijalizi cha aina ya kijalizo cha ‘ndi-kpt-o’. Knguvu kikiwa nguvu ya swali, kinaweza kuteua kijalizo ‘amba-kpt-o’ au ‘ndi-kpt-o’. Kwa upande mwingine Knguvu chenye neno kuu la nguvu urejesho huteua kijalizo ‘amba-kpt-o’.

### **Asili ya ‘kpt kijzo’ na utokeaji wake katika muundo wa sentensi**

Mbali na vijalizo changamano vilivyojadiliwa hapo juu, mifano ya 19b na 20a iliyorudiwa hapo chini kama 25a na b inaonyesha kuwa kiambishi cha ‘-o’ rejeshi (kpt kijzo) kinachotokea kama kiambishi katika vitenzi kinaweza kutumika kuchopoa viima na viambajengo vingine visivyokuwa viima katika sentensi za Kiswahili.

- 25a. Watoto walionunua mkate
  - b. Mkate walionunua watoto

Kutokana na data hii, tunaweza kusema kuwa kwanza, uchopoaji wa viambajengo kupitia ‘-o’ rejeshi (kpt kijzo) huzalisha vishazi virejeshi na pili kuwa kiambishi hiki kinaweza kitumika kuchopoa viima sawia na viambajengo vingine visivyokuwa viima katika lugha hii.

Aidha, ni dhahiri kuwa kpt kijzo kinaweza kutokea kama kiambishi awali ama kiambishi tamati kinapotumika kuchopoa viambajengo kama ilivyo katika vishazi virejeshi vifuatavyo:

- 26 a. [Nyumba inayojengwa] itabomolewa
  - b. [Nyumba ijengwayo] itabomolewa
- 27 a. Barua alizoandika mwalimu
  - b. Barua aziandikako mwalimu

Istoshe, kutokana na deta hii, inabainika kuwa kiambishi kpt kijzo hupatana na nomino inayochopolewa, iwe kiima au yambwa. Katika mifano ya 25 kwa mfano, kiambishi hiki kinapatana na kiima kilichochopolewa katika 25a huku kikipatana na yambwa iliyochopolewa katika 25b.

Masuala haya yote kwa ufupi yanazungukia mofolojia ya kpt kijzo cha Kiswahili. Katika sehemu inayofuata, nimetoa mwanga zaidi kuhusu maswala haya muhimu ya mofolojia ya kpt kijzo.

### **Mofolojia ya ‘kpt kijzo’ cha Kiswahili**

Viambishi virejeshi vimewahi kushughulikiwa na wanaismu kadhaa wakiwemo Wasike (2007) na Dierks (2010) ambao walichunguza kiambishi hiki katika lugha ya Kibukusu na Ashton na wengine (1954) ambao walichunguza kiambishi hiki katika lugha ya Kiganda. Ashton anarejelea kiambishi hiki kama vokali au irabu ya mwanzo kutokana na sababu kuwa kiambishi hiki hutokea kama irabu inayotangulia viambishi vingine vyote katika kitenzi cha kishazi kirejeshi kinachotokana na uchopoaji wa kiima. Hata hivyo, kiambishi hiki katika Kiswahili hakiwezi kurejelewa kama vokali ya mwanzo kwa sababu mbili:

- i) Ingawa kuna hali ambapo kiambishi hiki hutokea kama irabu pekee katika Kiswahili, si kila mara kiambishi hiki hutokea kama vokali peke katika lugha hii.

ii) Katika Kiswahili, kiambishi hiki hutokea baada ya viambishi vingine kama vile kiambishi kipatanishi kiima, kiambishi cha wakati ama hali na hata katika hali zingine, kiambishi hiki hutokea kama kiambishi tamati.

iii) Kiambishi hiki huwa na dhima tofauti kinapotokea kama kiambishi awali na kiambishi tamati.

Wasike naye amerejelea kiambishi hiki kama kiambishi kipatanishi cha viwakilishi viulizi kutokana na sababu kuwa ni kiambishi kinachopatanisha kiima kilichochopolewa ili kuunda sentensi ulizi kama ifuatayo:

28a. Naanu o-wa-lima kumukunda?

Nani kpt<sub>wh</sub>- kptK.wktlpt-mzz-IT shamba

Nani aliyelima shamba.

b. Nani waliokununulia nguo mpya?

Katika mfano wa 28a, kiambishi'-o-' kinarejelea kiwakilishi kiulizi 'naanu' (nani) ambacho kinatokea katika uwanja wa kijalizo na ambacho kinasababisha kishazi kizima kuwa na nguvu ya swali. Kwa vile, kiambishi hiki kinapatanishwa na kiwakilishi kiulizi 'naanu', Wasike anakirejelea kama kipatanishi cha wh-. Kifupisho wh- kwa maana ya viwakilishi viulizi sawia na viwakilishi viulizi vyta Kiingereza: who (nani), which (-pi), why (kwa nini) na where (wapi). Japo Kiswahili sawia na Kibukusu kina miundo inayotumia kiambishi cha '-o' rejeshi kama kiambishi kipatanishi kiulizi (yaani cha wh-) kama ilivyo katika sentensi ya 28b, sio kila mara kiambishi hiki hupatanishwa na KN kilichochopolewa chenye kubeba nguvu swali. Kwa mfano katika sentensi zifuatazo, KN vinavyopatanishwa na kiambishi '-o-' vinabeba nguvu vishazi tofautitofauti:

29 a. Watoto wanaοimba vizuri

b. Wanasiaya ndio watakaοsuluhisha tatizo hilo

Sentensi hizi mbili zinabeba nguvu vishazi tofauti zikiwemo: 29a kishazi kirejeshi na 29b kishazi teguzi arifu. Kutokana na uamilifu huu wa '-o-' rejeshi, hatuwezi kutoa hukumu ya jumla kuwa '-o-' rejeshi ni kipatanishi cha wh- kila mara. Huu upungufu wa ufasiri wa '-o-' rejeshi umetuelekeza kukirejelea hiki kiambishi kipatanishi kama kipatanishi kijalizo (kpt kijzo) kutokana na sababu kuwa kiambishi hiki hupatanisha kitende na nomino zilizochopolewa hadi katika ulingo wa Kkilzo au ukingo wa kushoto wa sentensi. Kwa misingi hii kwa hivyo, katika kazi hii, nitakirejelea kiambishi hiki kama 'kpt kijzo'.

Kiambishi kpt kijzo kinapotumika kuchopoa viambajengo, kitende katika muundo hudhihirisha upatanishi mara mbili: kwanza kati ya kitende na kiima kisha kati ya kiambajengo kilichochopolewa na kpt kijzo. Hali hii inaweza kuthibitika kupitia viambishi vilivyopigwa mstari katika mifano ya 29 hapo juu. Jedwali lifuatalo nalo linaonyesha kuwa kpt kijzo hubadilika kwa mujibu wa ngeli ya nomino inayochopolewa:

### Jedwali 2: Vipatanishi vijalizo vya Kiswahili

<b>Ngeli</b>	<b>Mifano ya nomino</b>	<b>Kiambishi vya nomino</b>	<b>Kiambishi kpt kiima-yambwa</b>	<b>Kiambishi kpt kijzo</b>
<b>1</b>	<b>mtoto</b>	<b>mu</b>	<b>a/mu</b>	<b>ye</b>
<b>2</b>	<b>watoto</b>	<b>wa</b>	<b>wa</b>	<b>o</b>
<b>3</b>	<b>mti</b>	<b>m</b>	<b>u</b>	<b>o</b>
<b>4</b>	<b>miti</b>	<b>mi</b>	<b>i</b>	<b>yo</b>
<b>5</b>	<b>jino</b>	<b>ji</b>	<b>li</b>	<b>lo</b>
<b>6</b>	<b>meno</b>	<b>ma</b>	<b>ya</b>	<b>yo</b>
<b>7</b>	<b>kitanda</b>	<b>ki</b>	<b>ki</b>	<b>cho</b>
<b>8</b>	<b>vitanda</b>	<b>vi</b>	<b>vi</b>	<b>vyo</b>
<b>9</b>	<b>nyumba</b>	<b>n</b>	<b>i</b>	<b>yo</b>
<b>10</b>	<b>Kuta, nyuzi</b>	<b>Ø/ n</b>	<b>zi</b>	<b>zo</b>
<b>11/14</b>	<b>Ukuta, uzi</b>	<b>u</b>	<b>u</b>	<b>o</b>
<b>15/17</b>	<b>kuimba</b> Shambani- kuna	<b>ku</b>	<b>ku</b>	<b>ko</b>
<b>16</b>	<b>Shambani - pana</b>	<b>pa</b>	<b>pa</b>	<b>po</b>
<b>18</b>	<b>Shambani - mna</b>	<b>mu</b>	<b>mu</b>	<b>mo</b>

Tukiangazia viambishi vibainishi vya ngeli na viambishi vipatanishi vinavyotokea kwenye vitenzi kiulinganishi, inabainika kuwa viambishi hivi havifanani moja kwa moja. Ngeli nyingi kama vile za 1, 3, 4, 5, 6, 9 na 10 zinachukua viambishi vipatanishi vilivyo tofauti kabisa na viambishi vya nomino katika ngeli husika. Kazi hii, inachukulia kuwa huu ni ushahidi muhimu kwamba upatanishi kati ya nomino na vitenzi huhusisha zaidi ya sifa za uwana (ngeli) ambazo zinabainika kuitia viambishi vya ngeli. Katika Kiswahili, ilibainika kuwa nomino hushiriki katika upatanishi kama KKIB na kuwa ukamilifu wa *phi* wa KKIB unahusisha sifa za idadi, uwana na nafsi. Tofauti zinazoshuhudiwa kati ya viambishi hivi kwa hivyo zinatokana na sifa zinazomilikiwa na viambishi husika. Viambishi vya ngeli humiliki sifa za ngeli pekee huku viambishi vya upatanisho vikimiliki sifa za idadi, uwana na nafsi. Swali ni je, upatanishi wa ‘kiima/yambwa’ una umuhimu gani katika kujadili viambishi vya o-rejeshi vinavyoshudiwa katika vitenzi vya vishazi virejeshi?

Uchunguzi wa mofolojia ya viambishi vya kpt kijzo vinavyodhiihirika, kiima kinapochopolewa ili kuunda vishazi virejeshi unaonyesha kuwa viambishi hivi vina uhusiano wa karibu sana na viambishi vipatanishi vya ‘kiima/yambwa’ kuliko viambishi vya ngeli vinavyotokea katika nomino. Hali hii inatuelekeza kuhitimisha kwamba mofolojia ya vitenzi vya vishazi virejeshi vinavyohusisha kpt kijzo hupatanishwa maradufu, kwanza na kiima cha kishazi husika kisha na kiambajengo kilichochopolewa.

Uchunguzi wa kiambishi kpt kijzo hushirikisha mofimu mbili; mofimu ya kwanza ikiwa ya upatanishi wa nomino iliyochopolewa huku ya pili ikiwa kiambishi ‘-o’ kisichobadilika. Mifano ifuatayo inabaini hali hii:

- 30a. Ngeli ya 1: a + o = ye
- b. Ngeli ya 2: wa + o = o
- c. Ngeli ya 3: u + o = o

- d. Ngeli ya 4: i + o = yo
- e. Ngeli ya 5: li + o = lo
- f. Ngeli ya 6: ya + o = yo
- g. Ngeli ya 7: ki + o = cho
- h. Ngeli ya 8: vi + o = vyo
- i. Ngeli ya 9: i + o = ye
- j. Ngeli ya 10: zi + o = zo
- k. Ngeli ya 11/14: u + o = o
- l. Ngeli ya 15/17: ku + o = ko
- m. Ngeli ya 16: pa + o = po
- n. Ngeli ya 18: mu + o = mo

Japo tumesema kuwa viambishi nya kpt kijzo vinavyoshuhudiwa katika vitenzi nya vishazi virejeshi vinavyotokana na uchopoaji vinajumuisha kiambishi kipatanishi na kiambishi cha ‘-o’ rejeshi, mifano katika 30 inaonyesha kuwa kpt kijzo kinachodhihirika huwa tofauti na ujumuisho wa moja kwa moja wa viwili hivi. Kwa mfano, katika mfano wa 30g, ujumuisho wa kiambishi ‘ki-’ na ‘-o’ unasitahili kubainika kama ‘kio’ badala ya ilivyo ‘cho’. Na hali ni hivi katika mifano mingine mingi katika huu mfano wa 30. Katika kuwajibikia hizi tofauti, tumerejelea mifanyiko ya kifonolojia. Ni desturi ya lugha za Kibantu kushuhudia mabadiliko sauti katika mipaka ya mofimu ambayo yanarejelewa kama mabadiliko ya kimofofonolojia. Mifano ya mabadiliko haya ni udondoshaji wa fonimu (30 b,e na f), uyeyusho (30 a, d na i), ukakaishaji (30 g) na mvutano wa irabu (30 a na i).

Kisha, ni nini uamilifu wa kiambishi ‘-o’ katika kpt kijzo?. Tunawaza kujadili uamilifu wa kiambishi ‘-o-’ kwa kuchunguza utokeaji wake katika vipashio vingine nya Kiswahili mbali na kpt kijzo. Mbali na kiambishi hiki kutokea katika vitenzi vyenye viambajengo vilivyochopelewa, kiambishi hiki hutokea katika vijalizo changamano ‘ndi-kpt-o’ na ‘amba-kpt-o’ vilivyojadiwa hapo juu pamoja na kwenye viashiria nya mbali kidogo kama ilivyo katika jedwali la 8 hapo juu. Katika hivi vipashio, kila kiambajengo huchukua kipashio ‘-o-’ sawia na kiambishi cha kpt kijzo kama iliyobainishwa katika mfano wa 30. Kiulinganishi, vipashio ‘ndi-kpt-o’, ‘amba-kpt-o’ na viashiria nya mbali kidogo, vyote hubeba dhana ya urejelezi. Wasike (2007) anasema kuwa viashiria kwa jumla huwa na sifa za kisemantiki za kuteua au kubainisha kitu kutoka kwa vingine vingi ulimwenguni. Kisintaksia, vipashio hivi hubainisha au kuteua kitu mahsusutu kutoka kundi kubwa, vinapotumika katika sentensi. Ni kwa misingi hii ndipo tunasema kuwa uamilifu wa kiambishi ‘-o-’, si katika vitenzi nya vishazi virejeshi pekee bali hata katika viashiria mbalimbali na vijalizo changamano, ni kubaini urejelezi. Vinginevyo kwa hivyo ni kuwa kiambishi hiki hukaribiana katika uamilifu na viwakilishi mbalimbali katika lugha hii kwani viwili hivi hurejelea kitu au nomino fulani dhahiri. Hitimisho hili linapatana na lile la Ashton (1945), Polome (1967) kuhusu kiambishi hiki katika Kiswahili, Austen (1974) katika Kibukusu na Nkemnji (1995) katika lugha ya Nweh. Kiambishi kpt kijzo ‘-o-’ aidha huwa na dhima ya unominishaji kinapotokea katika kitenzi kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

- 31a. Watoto wanacheza vizuri
- b. **Wanaocheza** vizuri...

Mfano wa 31a umehusisha kitenzi ‘wanacheza’ katika muundo wake. Katika mfano wa 31b, uambishi wa kpt kijzo umegeuza kitenzi cha muundo wa 31a kuwa kiwakilishi cha KN watoto katika huu mfano wa 31b. Kwa hivyo, kpt kijzo kina sifa za +nomino.

Tukiendelea na uchanganuzi wa mofolojia ya kpt kijzo, katika mfano wa 29a na b hapo juu, ilibainika kwamba kpt kijzo kinaweza kutokea kama kiambishi awali au kiambishi tamati. Katika mifano hii, japo nguvu kishazi (force) ya vishazi kirejeshi haiathiriki kwa mujibu wa nafasi ambamo kiambajengo hiki hutokea katika kitenzi, nafasi ya utokeaji wa kiambishi hiki kwa mujibu wa mzizi wa kitenzi huathiri dhana ya njeo (wakati/hali) ya sentensi husika. Hali hii inaweza kuwekwa wazi zaidi kwa kutumia sentensi za Kiswahili zenyenye hali na wakati pamoja na kpt kijzo kinachotokea kama kiambaishi awali na kiambishi tamati.

- 32i) a. Watoto walicheza
  - b. Watoto waliocheza
  - c.\*Watoto walichezao
- ii) a. Watoto wanacheza
  - b. Watoto wanaocheza
  - c.\*Watoto wanachezao
- iii) a. Watoto watacheza
  - b. Watoto watakaocheza
  - c.\*Watoto watachezao
- iv) a. Watoto wamecheza
  - b.\*Watoto wameocheza
  - c.\*Watoto wamechezao
- v) a. Watoto hucheza
  - f.\*Watoto huocheza
  - c.\*Watoto huchezao
- vi). Watoto wachezao

### Jedwali 3: Mtagusano kati ya viambishi virejeshi, wakati na hali

Nafasi ya tokeaji wa kirejeshi	Nyakati			Hali	
	uliopita	ulipo	ujao	timilifu	mazoea
Kiambishi awali	✓	✓	✓	*	*
Kiambishi tamati	*	*	*	*	*

\* Kiambishi cha ‘-o’ kirejeshi tamati hutokea tu katika kitenzi wakati ambapo hapana kiambishi chochote cha wakati au hali .

Data hii inazua kizungumkuti cha namna viambishi vya wakati na hali vinavyotagusana na viambishi vya kpt kijzo katika mofolojia ya vitenzi vya Kiswahili. Kama tulivyotaja awali, kiambishi kpt kijzo kinaweza kutokea kama kiambishi awali au kiambishi tamati. Ilivyo ni kuwa, kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi awali, kinaweza kutokea pamoja na kiambishi cha wakati kama ilivyo katika mifano ya 32 i, ii na iii lakini kamwe, kiambishi hiki hakiwezi kutokea pamoja na kiambishi cha hali kama ilivyo katika mifano ya 32 (iv – v) b. Kwa upande mwingine, kiambishi kpt kijzo hakiwezi kutokea pamoja na viambishi vya hali au njeo kinapotokea kama kiambishi tamati kama ilivyo katika mifano ya 32 (i – v) c.

Ili kufafanua zaidi kuhusu hali inayodhahirika katika mifano ya 32, ni muhimu kuchunguza mofolojia ya viambishi vya vitenzi vya Kiswahili kwa jumla. Kwa mujibu wa mofolojia ya

vitenzi vya Kiswahili, kitenzi huwa na mapengo 9 ya mofu mbalimbali. Pengo la 4 hujazwa na mofimu ama nyakati au hali na kwa hivyo viwili hivi haviwezi kutokea kwa pamoja katika kitenzi kimoja kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

- 33a.\*Wanafunzi walihuimba
- b.\*Watu wametaimba

Usosarufi wa sentensi hizi kutokana na sababu kwamba mofimu zilizopigwa mistari zinang'ang'ania nafasi moja ya pengo la 4 la viambishi vya vitenzi. Ili kukwepa huu mkinzano, lugha ya Kiswahili hutumia vitenzi visadizi ili kubainisha wakati na hali katika sentensi kama ilivyo katika mifano ifuatayo inayotokana na sentensi za 33 hapo juu:

- 34a. Wanafunzi walikuwa wakiimba
- b. Watu watakuwa wameimba

Mifano hii ina uhusiano na hali inayotokea katika sentensi za 32 (i –vi). Katika mifano hii ya 32, kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi awali, hakiwezi kamwe kutokea pamoja na kiambishi cha hali. Aidha kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi tamati cha kitenzi hakiwezi kutokea pamoja na viambishi vya wakati/hali.

Semantiki ya kitenzi chenye kiambishi kpt kijzo cha tamati inabaini kuwa kiambishi hiki hubeba dhana ya wakati uliopo, hali ya mazoea. Kwa hivyo, kiambishi hiki hakiwezi kutokea pamoja na viambishi vingine vya hali na wakati kwa sababu hali kama hii huweza kuleta mkinzano wa kisemantiki kama si uradidi. Kwa upande mwengine, mifano ya 32 inaonyesha kuwa kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi awali, kuna uwezekano wa kiambishi hiki kutokea pamoja viambishi mbalimbali vya wakati japo kiambishi hiki hakiwezi kamwe kutokea pamoja na kiambishi cha hali kama inavyobainishwa katika sentensi ya 32 (iv – v) b.

Pendekezo letu ni kuwa kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi awali katika kitenzi huwa kinabeba dhana ya hali. Na kwa hivyo, kiambishi hiki kina mofimu pacha za urejeshi na hali. Kutokea pamoja kwa kpt kijzo cha wakati pamoja na kiambishi cha hali kinasababisha ama mkinzano wa kisemantiki au uradidi. Ushahidi kuwa kiambishi kpt kijzo cha awali huwa na kiambishi cha wakati hutokana na hali kuwa kiambishi cha wakati, kpt kijzo cha awali na kiambishi cha hali hakiwezi kutokea kwa pamoja katika sentensi kama inavyobainishwa katika mifano ifuatayo:

- 35a.Watoto wanacheza
- b.\*Watoto wanahucheza
- c.Watoto huwa wanacheza
- d.\*Watoto huwa wanaocheza

Katika mfano wa 35b ni dhahiri kuwa kiambishi cha hali hakiwezi kutokea pamoja na kiambishi cha wakati katika kitenzi kimoja. Kama tulivyotaja awali, viambishi hivi hukalia pengo moja katika mofolojia ya vitenzi vya lugha hii. Ili wakati na hali vibainishwe, lazima kitenzi kisaidizi kinachotumika kama 'kapu' la kubeba njeo kiingizwe katika muundo kama ilivyo katika mfano wa 35 c. Hata hivyo, licha ya haya yote kutokea katika mfano wa 35d, usosahihi wa sentensi hii haukulaliki. Huu ni ushahidi kuwa kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi awali huwa tayari kina kiambishi cha mazoea. Machukulizi haya

yanajumlishwa kwa vitenzi vingine vinavyochukua viambishi nya wakati uliopita na ujao pamoja na kiambishi kpt kijzo cha awali japo si dhahiri katika hali hii iwapo kiambishi kpt kijzo cha awali kinachotokea pamoja na viambishi nya wakati uliopita na ujao hubeba vilevile mofimu ya hali ya mazoea kama ilivyo katika wakati uliopo au mofimu nyingine tofauti ya hali. Utafiti huu umewachia jukumu hili tafiti zingine za baadaye katika nyanja hii.

Kwa muhtasari, sehemu hii imejedili masuala ya mofolojia ya kpt kijzo. Miongoni mwa masuala muhimu yaliyoibuka ni kuwa:

- i. Kitenzi chenye kuchopoa viambajengo vyake kuptit kpt kijzo hudhihirisha upatanishi maradufu: moja na kiima katika muundo na kisha na kiambajengo kilichochopolewa kiwe kiima au yambwa.
- ii. Kiambishi kpt kijzo huathirika na mifanyiko mbalimbali ya kimofofonolojia.
- iii. Kiambishi kpt kijzo hutokea kama kiambishi awali na vilevile kiambishi tamati katika mofolojia ya vitenzi. Nafasi ya utokeaji wa kpt kijzo katika kitensi hutegea utokeaji wa viambishi vingine nya wakati na hali.
- iv. Kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi tamati huwa ni mofimu pacha ya hali ya mazoea na urejelezi na kwa hivyo kamwe kiambishi hiki hakiwezi kutokea pamoja na viambishi nya wakati au hali.
- v. Kiambishi kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi awali, kiambishi hiki huwa na mofimu fulani ya hali na kwa hivyo kiambishi hiki hakiwezi kutokea pamoja na viambishi vingine nya hali japo kinaweza pamoja na kiambishi cha wakati.

Baada ya kubaini mofolojia ya kiambishi kpt kijzo, ni muhimu kushughulikia miundo ya sentensi zenye kiambishi kpt kijzo.


### **Nafasi ya kpt kijzo katika Muundo wa Sentensi ya Kiswahili**

Swali lingine muhimu kuhusu mofosintaksia ya kpt kijzo ni je, katika vishazi au sentensi zinazochopoa viambajengo, kiambajengo hiki hukalia nafasi gani katika muundo? Sehemu hii, imezingatia muundo wa vishazi virejeshi vinavyotumia mbinu ya kpt kijzo kuchopoa viambajengo vyake, kwa lengo la kuonyesha namna kiambishi hiki hujikuta miongoni mwa viambishi nya vitenzi na kuwajibikia upatanishi maradufu kati ya kiima na vitenzi katika miundo hii. Maeleo ambayo tulitoa katika sehemu ya 1.4.1 yanazua masuala yafuatayo muhimu ambayo lazima yawajibikiwe kimuundo:

- i. Nini nafasi ya uingizaji wa kpt kijzo katika muundo wa kishazi kirejeshi?
- ii. Tunawajibika vipi hali ambapo kiambishi kpt kijzo katika Kiswahili kinaweza kutokea kama kiambishi awali na kiambishi tamati?
- iii. Tunawajibikia vipi upatanishi maradufu unaoshuhudiwa katika vitenzi nya vishazi virejeshi vichopoaji kiima?

Kama tulivyotaja hapo juu, mofolojia ya kpt kijzo cha Kiswahili inajumuisha kiambishi kipatanishi cha KN kilichochopolewa pamoja na kiambishi ‘-o’ cha urejeshi. Katika kushughulikia swali la kwanza, tutachukulia kuwa sentensi ya kauli kama ya 19a ambayo imerudiwa kama ya 36 hapo chini ina muundo ufuatao wa 37 wa kidesturi ambapo kiima hutua katika nafasi ya Kib cha Kwkt na kuingia upatanisho na kitensi:

## 36. Watoto walinunua mkate




Hata hivyo, uwakilishaji wa vishazi kirejeshi kama kile cha 19b ambacho kitenzi chake kina kpt kijzo kina utata hasa ikizingatiwa kuwa kishazi hiki kina viambajengo vinavyotokea katika mawanda ya kijalizo. Kabla ya kushughulikia hiki kiambishi kpt kijzo, kwanza hebu tuchunguze namna vishazi virejeshi nya aina hii nya lugha ya Kibukusu vimewahi kuchanganuliwa ili tujenge uchanganuzi wetu kwa msingi huu. Katika Kibukusu, ni muhimu kutambua kuwa kpt kijzo (kinachowezesha uchopoaji wa kiima kama ilivyo katika mfano wa 38) ni sahihi kikilinganishwa na kile cha Kiswahili ambacho kinaundwa kutokana na mofimu mbili.

38. Ba-ba-ana ba-ba-akwa....

N2 - N2-toto kpt kijzo-N2-anguka  
Watoto walioanguka...

Katika Kibukusu, sawia na Kiswahili, kitenzi katika kishazi kirejeshi hudhihirisha upatanishi mara mbili. Katika hali hii, kiambishi cha kwanza huwa kiambishi kpt kijzo huku kiambishi cha pili kikibainisha upatanishi wa kidesturi wa kiima-kitenzi. Muundo uliosahilishwa wa kishazi cha 38 kwa mujibu wa Wasike (2007: 29) ni ufuatao:

## 39.



Katika muundo huu, inachukuliwa kuwa katika 'kishazi kirejeshi kichopoaji kiima' cha Kiswahili, neno kuu la Kukomo yaani ukomo huwa tupu kifonolojia na kuwa Kib cha neno kuu hili (ukomo) lina sifa dhabiti ya kiima ambalo linaweza kuhakikishwa tu na kiima. Hali hii

inamaanisha kuwa katika ‘kishazi kirejeshi kichopoaji kiima’, nafasi ya Kib cha Kukomo imetengewa kiima.

Kwa hivyo, katika uundaji wa kishazi kirejeshi kiima, kwanza kiima huingia katika upatanishi na kitenzi kilichosogea kutoka katika KT hadi wkt huku kiima kikiwa kimesogea kutoka Kt hadi Kib cha Kwkt. Kupitia upatanishi wa kuelekea juu, upatanishi wa kwanza unatokea ambapo kitenzi kinapatana na kiima kama kinavyobainishwa na mshale wa kwanza. Hatua ya pili ni kuwa kutokana na sifa ya wakati ya ‘ukomo’, kitenzi kinasogea hadi kwenye neno kuu la Kukomo katika mawanda ya kijalizo. Katika hii hatua ya pili, kiima nacho kinasogea hadi Kib cha Kwkt kutokana na sifa dhabit za ukomo. Ni katika hali hii ndipo upatanishi wa pili unaobainika kwenye vitenzi virejeshi unatokea. Huu upatanishi wa pili ndio unaosababisha kitenzi kuonekana kuwa na upatanishi mara mbili. Kipatanishi cha pili ndicho kinachorejelewa kama kpt kijzo.

Ingawa muundo wa 39 unaonekana kuwajibikia upatanishi maradufu unaoshuhudiwa katika vishazi kirejeshi cha Kibukusu, muundo sawa na huu hauwezi kuwajibikia vishazi virejeshi vichopoaji viima kama vile vya 38a na b hapo chini kwa sababu:

- i. kpt kijzo cha Kiswahili ni chamgamano kwa vile kinajumuisha kiambishi kipatanishi cha nomino iliyochopelewa na kiambishi cha –o- rejeshi kinyume na kile cha Kibukusu ambacho ni sahili.
- ii. kpt kijzo cha Kibukusu hutokea kama kiambishi awali cha kwanza katika kitenzi huku kpt kijzo cha Kiswahili kikitokea kama kiambishi awali kinachotokea baada ya viambishi vingine au kama kiambishi tamati.


Hizi ni tofauti muhimu ambazo lazima ziwajibikiwe kimuundo. Kuna baadhi ya wanaismu ambao wamewahi kushughulikia kpt kijzo chenyе mofolojia changamano kama kpt kijzo cha Kiswahili. Henderson (2005) na Kula 2004, mbali na kukitambua kiambishi hiki kama Kirai kirejeshi ( $K_{Kirejeshi}$ ), wanaismu hawa hawakukijadili zaidi ili kuonyesha uamilifu wake wala nafasi yake katika muundo wa vishazi virejeshi katika lugha hizi. Wasike (2007) anasema kuwa dhima ya kiambishi hiki katika lugha zote zinazomiliki kiambishi hiki ni kutambulisha kishazi husika kama kishazi kirejeshi. Ngonyani (1999), Buell (2002), na Henderson (2005) walijaribu kushughulikia kiambishi cha –o- rejeshi kinachotokea katika sentensi kama ya 40a na b hapo chini.

- 40a. Barua alizoandika mwalimu
- b. Barua aziandikazo mwalimu

Kulingana na Ngonyani, Buell na Henderson, kiambishi cha –o-rejeshi huingizwa katika muundo kama neno kuu la Kukomo na kuwa kitenzi husogea hadi sehemu hii ili kutoa uwenyeji kwa kiambishi –o- ambacho hakiwezi kutokea kifolojia kama faridi peke. Kiima kwa upande mwengine husogea hadi nafasi ya Kib cha Kukomo kutokana na sifa thabiti ya kiima ya ukomo. Ni katika hali hii ndipo kiambishi hiki huingia katika upatanishi na kiima kupitia upatanishi wa kuelekea juu.

Muundo uliosahilishwa wa sentensi hizi za 40a na b ukiwa ufuatao wa 41, mishale ikitumika kuonyesha namna kitenzi hujikuta kimepatanishwa mara mbili, kwanza na kiima kisha na KN kilichochopolewa:

41.



Licha ya maelezo haya, kufafanua namna mpangilio wa viambajengo unavyotokea katika vishazi virejeshi hivi, muundo huu unakabiliwa na upungufu mbalimbali. Kwanza ni kuwa ni dhahiri kuwa katika mifano ya 40a na b, kpt kijzo kinaweza kutokea kama kiambishi awali au kiambishi tamati. Hata hivyo, muundo wa 41 unaonua kuonyesha miundo ya sentensi za 40a na b haiwajibikii hizi nafasi tofauti tofauti ambazo kpt kijzo huweza kutokea katika kitenzi cha kishazi cha Kiswahili kilichochopoa viambajengo vyake .

Pili, data zingine za lugha hii zinapochunguzwa, zinabaini udhaifu zaidi wa pendekezo hili la wanaismu Ngonyani, Buell na Henderson. Mifano ifuatayo inatoa ushahidi kinyume kuwa kiambishi cha -o- rejeshi huingizwa katika muundo katika ulingo wa Kkijzo.

42a. soma kama [wanavyotaka walimu]


b. soma kama [walimu wanavyotaka]

43a.[alipoondoka Juma]

b. [Juma alipoondoka]

Vishazi virejeshi katika sentensi za 40 na 41 (ambavyo vimewekwa katika mabano) vinafanya kazi ya vielezi vya namna na wakati mtawalia. Katika vishazi virejeshi vya 42a na 43a kitenzi kimenyanyuka hadi katika nafasi ya Kkilzo na kusababisha mpinduo wa kitenzi ambaa unawezesha kiima kuja baada ya kitenzi. Kwa mfano, muundo wa 44a uliosahilishwa utakuwa ufuataao:

44.



Licha maelezo haya kudhahirisha kikamilifu, ukweli kuwa kiambishi kpt kijzo huingizwa katika muundo katika nafasi ya Kukomo na kuwa kitenzi katika muundo hupinduliwa ili kutoa uwenyeji kwa hiki kiambishi kpt kijzo, vishazi virejeshi vya 42b na 43b vinaonyesha ushahidi kinyume. Katika mifano hii, imebainika kuwa mpinduo wa kitenzi unaoshuhudiwa katika


mifano ya 42a na 43a ni wa hiari. La muhimu kwa ushahidi wetu ni kuwa licha ya kutopinduliwa kwa kitenzi, vitenzi katika miundo hii bado vina viambishi vya kpt kijzo. Huu ni ushahidi muhimu dhidi ya pendekezo kuwa kiambishi cha -o- rejeshi hakiingizwi katika muundo katika nafasi ya Kukomo katika kiwango cha Kkijzo. Aidha ushahidi huu unaenda kinyume na pendekezo la Ngonyani (1999), Buell (2002), na Henderson (2005) kuwa kitenzi katika kishazi kama vile vishazi virejeshi hupinduliwa ili kitoe uwenyeji kwa kpt kijzo ambacho hakiwezi kutokea kama faridi peke. Imebainika kuwa mpinduo wa kitenzi husababishwa na hitaji lingine huru lisiloegemea kiambishi cha -o- rejeshi.

Ushahidi mwingine muhimu zaidi dhidi ya dhana kuwa kitenzi hupinduliwa hadi nafasi ya kijalizo katika vishazi virejeshi (ili kutoa uwenyeji kwa kiambishi kpt kijzo kinachoingizwa katika muundo kama neno kuu la Kukomo) unatokana na kishazi kirejeshi cha vitenzi vya wakati ukomo mwambatano kama ilivyo katika mifano ya 45a na b hapo chini. Vitenzi vya wakati ukomo mwambatano hujumuisha kitenzi kikuu na kisaidizi ambavyo huwa na viambishi vya wakati na kwa hivyo videnzi hivi vyote huingia katika upatanishi na kiima katika muundo. Kwa mfano:

- 45 a. Juma alikuwa anasoma kitabu
- b. Kitabu<sub>k</sub> (alichokuwa anasoma), Juma t<sub>i</sub> t<sub>k</sub>
- c.\*Kitabu<sub>k</sub> alichokuwa<sub>i</sub> Juma t<sub>i</sub> anasoma t<sub>k</sub>

Katika mifano hii, sentensi ya 45a ni mfano wa sentensi ya wakati ukomo mwambatano. Kishazi cha 45b nacho ni kishazi kirejeshi kinachotokana na sentensi ya 45a. KN 'kitabu' cha 45a kimechopolewa kutoka katika nafasi ya yambwa hadi kwenye ulingo wa Kkijzo na kusababisha kishazi kizima kubainika kama kishazi kirejeshi. Aidha, kishazi kirejeshi kinafikiwa kupitia kupinduliwa kwa kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi kutoka katika kiwango cha Kwkt hadi kwenye ulingo wa Kkijzo. Mfano wa 45c, unaonyesha kuwa lazima videnzi hivi vipinduliwe kwa pamoja na kwa hivyo hali ambapo kitenzi kikuu pekee kinapinduliwa inasababisha usosarufi. Kama ingekuwa kweli kwamba kupinduliwa kwa kitenzi katika sentensi ya 45b kunatokana na haja ya kutoa uwenyeji kwa kiambishi kpt kijzo, tungetarajia kishazi cha 45c, ambacho kitenzi cha juu pekee kimepinduliwa ili kutoa uwenyeji kwa kpt kijzo, kikubalike kisarufi. Kukataliwa kwa kishazi cha 45c na kukubalika kwa kishazi cha 45b kuna maana kuwa usogezi wa kitenzi hadi ulingo wa Kkijzo katika vishazi hivi huenda: i. hauhamashwi na haja ya kutoa uwenyeji kwa kiambishi kpt kijzo ambacho kinasemekana huingizwa katika muundo katika nafasi ya kijalizo na ii. unaashiria kuwa viambajengo vinavyosogezwa hadi kwenye Kkijzo katika sentensi kama hii huwa ni vipashio vikubwa kuliko videnzi.

Ili kukabiliana na huu upungufu wa pendekezo la Ngonyani, Buell na Henderson, tutafuata mwelekeo wa fikira wa Wasike (2007) kwamba kiambishi cha kpt kijzo cha Kiswahili huingizwa katika muundo katika nafasi ya Kwkt kabla ya kitenzi kusogea hadi kwenye ukingo wa kushoto mwa kishazi kirejeshi. Kulingana na Wasike, kiambishi hiki huingizwa katika muundo kama neno kuu la kirai kirejeshi (K<sub>Kirejeshi</sub>). Kwa hivyo, miundo ya kishazi kirejeshi cha 40a utakuwa ufuata:




Katika mfano huu, kpt kijzo hutokea kama kiambishi awali kitenzi. Ili kuwajibikia hali hii, kama tulivyotaja, kiambishi kpt kijzo huingizwa katika muundo kama neno kuu la  $K_{Kirejeshi}$ . KN ‘barua’ ambacho kinapatanishwa na kpt kijzo nacho huingizwa katika muundo katika nafasi ya Kt na kusogea hadi nafasi ya Kib cha  $K_{Kirejeshi}$  ambapo upatanishi unatokea kati yake na -o- rejeshi. Zao la upatanishi huu linatokea kuwa kiambishi kpt kijzo ‘z-o’. Kisha kitenzi kinanyanya kwanza hadi kwenye neno kuu la ‘-o- rejeshi’ na kisha, pamoja na kpt kijzo, viwili hivi vinasogea hadi kwenye wkt kupitia usogezi wa neno kuu hadi neno kuu. Kitensi kinaposogea hadi kwenye  $K_{Kirejeshi}$ , kpt kijzo hujiambisha kwenye kitensi kama kiambishi awali kisha viwili hivi vinaposogea hadi kwenye Kwkt hujiambisha kulia mwa neno kuu la Kwkt ambalo katika hali yetu ni kiambishi cha wkt uliopita ‘-li’. Baadaye, KN ‘mwalimu’ kikiwa kiima, husogea kutoka nafasi ya Kib cha Kt hadi nafasi ya Kib cha Kwkt kutokana na KMZ ya wkt. Hatimaye, upatanishi unapotokea kati ya wkt na kiima, kiambishi cha upatanishi kiima kinatokea kama kiambishi awali kinachotangulia viambishi vingine vyote katika kitensi. Matokeo ya mchakato huu wote ni neno kuu la Kwkt linalodhiihikira kimofolojia kama ‘alizoandika’.

Hatua ya mwisho, ni usogezi wa viambajengo hadi katika uwanja wa kijalizo kama inavyoonyeshwa na mishale juu zaidi. Katika hatua hii, kutokana na sifa za urejeshi wa kitensi, kiambajengo changamano ‘alizoandika’ kinasongea hadi kwenye mchomozo wa Kukomo kilicho katika ulingo wa Kjilzo. Katika usogezi huu, kiambajengo ‘alizoandika’ hakisogei kama neno kuu bali kirai kilichonominishwa. Kwa hivyo kiambajengo hiki kinasogea hadi nafasi ya Kib cha Kukomo kama kiwakilishi, sawia na kiwakilishi kirejeshi ‘who’ cha Kiingereza. Hatimaye, KN ‘Barua’ kinasogea kutoka Kwkt hadi kwenye Kib cha KX. KX katika kishazi kirejeshi kama hiki huaminika kuwa na dhima ya kubainisha aina ya kishazi. KX katika kishazi

kirejeshi kwa hivyo ni sawa na Knguvu chenyeneno kuu ‘nguvu’ ambalo vilevile ni tupu kifonolojia na lenye uamilifu wa kubainisha kishazi husika kama kile cha aina ya kishazi kirejeshi.

Ufafanuzi huu, unawajibikia namna kpt kijzo katika Kiswahili hujikuta kikitokea kama kiambishi awali katika mofolojia ya kitenzi. Swali ni je, ni vipi tutawajibikia namna kpt kijzo hutokeea kama kiambishi tamati katika mofolojia ya vitenzi kama ilivyo katika mfano wa 40b? Ili kutofautisha sentensi ya 40a kutoka sentensi ya 40b, nimependekeza muundo ufuatao kwa sentensi ya 40b:



Tuliposhughulikia mofolojia ya kpt kijzo cha Kiswahili katika sehemu ya 1.4.1 hapo juu, tulifikia hitimisho kuwa kiambishi hiki kinapotokea kama kiambishi tamati huwa ni mofimu pacha ya hali ya mazoea na urejelezi na kwa hivyo kamwe kiambishi hiki hakiwezi kutokea pamoja na viambishi vya wakati au hali. Kwa hivyo, kiambishi hiki huingizwa katika muundo katika nafasi ya  $K_{\text{Kirejeshi}}$  lakini baada ya kuchomoza Kwkt, kiambishi hiki husogea kutoka nafasi yake ya  $K_{\text{Kirejeshi}}$  hadi kwenye wkt kufanya kazi kama neno kuu la kirai hiki kutokana na mofimu ya hali ya mazoea ambayo humilikiwa na kiambishi cha kpt kijzo kinapotokea kama kiambishi tamati. Kitenzi kinaposogea kutoka katika Kt hadi kwenye  $K_{\text{Kirejeshi}}$  kisha kwenye Kwkt, katika wkt, kitenzi katika muundo hujambisha kushoto mwa kpt kijzo ambacho huwa kimetangulia kitenzi katika utuaji katika sehemu hii. Hatimaye hatua zingine huendelea sawia na ilivyo katika muundo wa 44 unaowakilisha mfano wa 40a.

### **Hitimisho**

Kazi hii imeshughulikia sintaksia ya kirai kijalizo na uchopoaji wa viambajengo katika Kiswahili. Imebainika kuwa kuna haja ya kupanua zaidi virai vya kidesturi vinavyotokea katika kiwango cha ukingo wa kushoto wa sentensi ya Kiswahili ili kutoa nafasi ya utuaji wa vipashio vilivyocho polewa. Kazi hii imependekeza vipashio ziada vya: Kirai arifu na Kirai kiwakilishi. Katika kazi hii vilevile imedhihirika kuwa Kiswahili hutumia mbinu kadhaa kuchopoa

viambjengo vyake, zikiwemo: kijalizo amba-o, kijalizo ndi-o na kpt kijzo -o-. Katika muundo wa sentensi chopozi, vijalizo amba-o na ndi-o, amba- na ndi- hutokea kama maneno makuu ya Kirai arifu huku kpt-o kikitokea kama neno kuu la Kirai Kiwakilishi. Kwa upande mwagine, kpt kijzo -o- huingizwa katika muundo katika kiwango cha Kwkt kama neno kuu la Kirai Kirejeshi, na baada ya kuingia katika upatanishi na kiima katika muundo, hutafuta wenyiji katika kitenzi kwenye muundo. Hatimaye, kitenzi chenye kipatanishi kijalizo hunyanyuliwa hadi katika nafasi ya Kkijzo ambapo kitenzi hiki hutokea kama kibainishi cha Kukomo.

## Marejeo

- A Dictionary of Linguistics and Phonetics (2008), 6<sup>th</sup> Ed.
- Diercks, M., (2010). *Agreement with Subjects in LuBukusu*. PhD Dissertation. Georgetown University.
- Taraldsen, C., (2001). Subject extraction, the distribution of expletives and stylistic inversion. In *Inversion in Romance and theory of universal grammar*, ed, by A. Hulk and J-Y. Pollock. Oxford: Oxford University Press.
- Ashton, (1945). *A Luganda Grammar*. London : Longmans, Green.
- Austen, (1974). Aspects of Bukusu syntax and phonology. PhD dissertation. Indiana
- Boskovic, Z., (2007). On the locality and motivation of Move and Agree :An even more minimal theory. *Linguistic Inquiry* 38:589-644.
- Boskovic, Z., (2008). *On Successive Cyclic Movement and the Freezing Effect of Feature checking*, In Sounds of Silence: Empty Elements in Syntax and Phonology, ed by J. Hartmann, V. Hegedus, H. Van Riemsdijk, 195-233. Amsterdam Elsevier.
- Bresnan, J., (1977). "The variables in theory of transformations" in Peter W Colicover, Thomas Wasow and Adrian Akmajian eds, papers from the MSSB-UC Irvine conference on the formal syntax of natural languages, 157-96, Academic press.
- Buell, L., (2002). Swahili amba-less clauses without head movement. UCLA working papers in African Linguistics 2, 86 – 106, No. 8 UCLA In Working Paper in Linguistics
- Cardinaletti, A., ( 2004). Towards a Cartography of Subjects Position.In the structure of CP and IP, edited by Luigi Rizzi, 115-165. New York:Oxford University Press
- Chomsky, N.,(2000). *Minimalist Inquiries: The Framework. Step by Step: Essays on Minimalist Syntax in honor of Howard Lasnik*. Martin, D. Michaels and J. Uriagereka (eds). Cambridge, Mass: MIT Press.
- Fox, D, (1999). *Economy and Semantics Interpretation*. Cambridge: MIT Press.
- Henderson B. (2005). The case for concord: the multiple agreement in Bantu in the proceedings of the 36<sup>th</sup> Annual meeting on the North East Linguistic society (NELS 36<sup>th</sup>) Amherst, MA.
- Palome, E., (1967). *Swahili Language Handbook*, Washington DC Center of Linguistics.
- Perlmutter, (1971). *Deep and surface structure constraints in syntax*. New York: Holt Rinehart and Winston.
- Perlmutter, (1986). *Deep and surface structure constraints in Syntax*. Doctorial dissertation, Massachusetts Institute of Technology.
- Radford, A., (2009). *Analyzing English sentences: A Minimalist Approach*. Cambridge University Press New York.
- Reinhart.A.,(2006). *Interface Strategies: Optimal and costlu Computations*. Cambridge: MIT Press.
- Richards, L. (2001). *Movement in Language Interactions and Architecture*, Oxford University Press.
- Rizzi, L & Shlonsky,( 2007).On some properties of CriterialFreezing. In CISL working papers on language and cognition, Vol 1, edited by V.Moscati, 145-158. Interdepartmental Centre for Cognitive Studies of Language, University of Sienna.
- Rizzi, L., (1997). 'The Fine Structure of the Left Periphery' In *Elements of Grammar*, edited by Haegeman,L. 281-337. Dordrecht: Kluwer Academic Publishers.

- Rizzi, L.,(2004).‘Locality and left periphery’, in A Belleti (ed.) *Structures and Beyond: The cartography of syntactic structures*, vol III, Oxford University Press,pp.223-251.
- Rizzi, L.,(2006). ‘On the form chains.Criterial positions and ECP effects in Cheng and Corver 2006, pp 97-133
- Wasike, A, (2007).The left periphery wh-in-situ and A- bar movement in Lubukusu and other Bantu languages.phD dissertation, Cornell University.
- Waxler & Culicover, (1982). *Formal Principles of Language Acquisition*. Cambridge, MIT Press.